

## Ujumbe kutoka ICPCN

1. Kila mtoto ana haki ya kupata huduma bora ya afya ikiwa ni pamoja na tibashifa.
2. Ni haki ya kila mtoto kupata matibabu bora ya maumivu na dalili za maradhi kwa kutumia dawa maalumu za watoto kila inapohitajika.
3. Huduma ya Afya kwa Wote Duniani ni sharti ijumuishe tibashifa kwa watoto na inafaa kutolewa na wahudumu wa afya waliohitimu.

*Kwa madhumuni ya ujumbe huu, neno 'mtoto' linamaanisha watoto wachanga, vijana wadogo na watu wa umri wa makamo katika kila nchi ulimwenguni ikiwa ni pamoja na waliofukuzwa makwao, walioadhiriwa na vita na dhuluma nyinginezo za kibinadamu; 'tibashifa kwa watoto' ni huduma maalumu itakayotolewa na wahudumu wa afya waliohitimu.*

## Maelezo

Tibashifa huboresha maisha ya mtoto kupitia udhibiti na upunguzaji maumivu unaofaa hasa kutokana na dalili za maradhi zinazosababisha dhiki. Kwa kufanya hivyo tibashifa vilevile humpa mtoto pamoja na familia yake malezi kamilifu. Tibashifa inafaa kuanza kupewa mtoto wakati wa uchunguzi na kuendelea hadi wakati wa matibabu kwa lengo la kumponya mtoto huyo. Inampa nguvu mtoto na familia yake baada ya kifo na hata katika kipindi cha kuomboleza. Tibashifa kamilifu hutumia mali na vifaa vinavyopatika katika mazingira husika na hutolewa na vikundi vya wauguzi waliohitimu. Mtoto anaweza kupewa huduma hiyo mahali popote ikiwa ni pamoja na nyumbani anakoishi<sup>i</sup>.

Matokeo ya utafiti uliofanywa na shirika la kimataifa linaloshughulikia tibashifa kwa watoto (ICPCN) yanaonyesha kwamba zaidi ya watoto milioni 21 duniani wanahitaji tibashifa. Wengi wao (98%) wanaishi katika mataifa maskini huku takriban nusu yao wakiishi barani Afrika<sup>ii</sup>.

### 1. Kila mtoto ana haki ya kupata huduma bora ya afya ikiwa ni pamoja na tibashifa.

Shirika la ICPCN linaamini kuwa tibashifa ni haki ya mtoto yeyote ambaye anaogua ugonjwa unaopunguza au kuhatarisha maisha yake. Imani hii inaungwa mkono na Sheria ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto, ambayo inaeleza kuwa uhusiano wowote na mtoto unafaa kuwa ule unaozingatia manufaa ya mtoto huyo<sup>iii</sup>. Sheria hii pia inaeleza tibashifa kuwa mojawapo ya haki za afya kwa mtoto<sup>iv</sup>.

Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Kibinadamu vilevile inatambua tibashifa kwa watoto kuwa sehemu muhimu sana ya huduma za afya na ambayo inafaa kutolewa na wataalamu waliohitimu<sup>v</sup>.

Katika Uamuzi wake wa 67.19 wa mwaka wa 2014, Baraza la Afya Duniani linayataka mataifa kujumuisha tibashifa katika mifumo yao ya kitaifa na kuhakikisha kuwepo kwa dawa za kuthibiti maumivu kama vile opioids ili kukabiliana na maumivu na dalili nyinginezo za maaradhi miongoni mwa watoto<sup>vi</sup>.

## **2. Ni haki ya kila mtoto kupata matibabu bora ya maumivu na dalili za maradhi kwa kutumia dawa maalumu za watoto kila inapohitajika.**

Maumivu ndio dalili ya maradhi iliyoenea sana na huathiri asilimia themanini (80%) ya watoto wanaougua saratani, asilimia sitini na saba (67%) ya wanaougua magonjwa yenye tiba na asilimia hamsini na tano (55%) ya wanaougua UKIMWI<sup>vi</sup>. Uzoefu wetu unaonyesha kuwa maumivu miongoni mwa watoto hayatibiwi inavyofaa kwa sababu ya ukosefu wa wataalamu wa kukadiria maumivu kwa mtoto na pia hofu ya wataalamu wa afya kutumia dawa za opioids. Mara nyingi Morphine ndiyo dawa inayotumiwa kupunguzia maumivu makali hasa ile ya kumeza kwani hiyo ni salama na haina gharama kubwa. Njia iliyopendekezwa na WHO inafaa kutumiwa kama mwongozo na kwamba dawa zinafaa kutumiwa kwa viwango vinavyoambatana na dawa maalumu za watoto.

Dalili nyinginezo pamoja na uchungu wa kisaikolojia na kiimani zinafaa kuthibitiwa inavyofaa ili kuhakikisha utulivu na hali nzuri ya maisha kwa mtoto pamoja na familia yake.

## **3. Huduma za Afya kwa Wote Duniani ni sharti ijumuishe tibashifa kwa watoto na inafaa kutolewa na wahudumu wa afya waliohitimu.**

Shirika la Afya Duniani<sup>viii</sup> linaeleza Huduma za Afya kwa Wote Duniani (UHC) kuwa hali ya watu wote kupata huduma za uboreshaji, matibabu, ubadilishaji hali na tibashifa kama wanavyozihitaji na kwamba huduma hizo zinafaa kuwa zenye gharama ya chini na ubora unaofaa ili kutimiza lengo lake. Hivyo basi tunasihhi kila serikali kuhakikisha kuwa tibashifa kwa watoto imepewa nafasi muhimu katika UHC.

<sup>i</sup> World Health Organization 2002

<sup>ii</sup> WPCA and WHO, Global Atlas of Palliative Care at End of Life, London, 2014.

<sup>iii</sup> UNCRC article 3

<sup>iv</sup> UNCRC, General Comment No 15, 2013

<sup>v</sup> Report of the UN Special Rapporteur on torture and other cruel or degrading treatment or punishment, March 2015

<sup>iv</sup> WHA Resolution "Strengthening of palliative care as a component of care throughout the life course,"

<sup>vii</sup> Ibid , p 95

<sup>viii</sup> World Health Organization [http://www.who.int/health\\_financing/universal\\_coverage\\_definition/en/](http://www.who.int/health_financing/universal_coverage_definition/en/)